

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu: "TAMISEMI"
Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420
Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013
Baruapepe: ps@poralg.go.tz



Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
Jengo la Mkapa,
2 Barabara ya Hospitali,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

TANGAZO LA KURIPOTI KAZINI

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inawatangazia Madaktari wote waliopata ajira ya Serikali na kutangazwa kupitia tovuti ya OR TAMISEMI tarehe 28/04/2017 na kutakiwa kuripoti OR TAMISEMI - Dodoma kwa ajili ya mafunzo ya awali na ukaguzi wa vyeti yaliyopangwa kufanyika tarehe 08 -10/05/2017, mnajulishwa kuwa mafunzo hayo yameahirishwa kwa muda hadi hapo mtakapo tangaziwa.

Mnaelekezwa kuwa mnatakiwa kuripoti katika vituo vyenu vya kazi kama ilivyopangwa katika orodha ya awali kabla au ifikapo tarehe 05/05/2017.

Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatakiwa kuwasilisha taarifa ya Madaktari wote walioripoti katika maeneo yao ifikapo tarehe 08/05/2017.

Hakikisha umeripoti na vyeti vyako halisi vya shule na taaluma ili kuepuka usumbufu. Orodha ya majina na vituo vya kazi inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa anuani ya www.tamisemi.go.tz na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa anuani ya www.moh.go.tz

OR TAMISEMI inaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza

Limetolewa na
Katibu Mkuu,
OR-TAMISEMI
01/05/2017